# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**JUNI, 2024**



**Mhe. Omar Said Shaaba**
**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda**



**Ndg.  Fatma Mabrouk Khamis**
**Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda**



**Dkt Said Seif Mzee**
**Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda**

## YALIYOMO

**1.0. UTANGULIZI........................................1**
**2.0. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA ........................................................4**
**3.0. MWENENDO WA BIASHARA....................5**
3.0.1. Hali ya Uchumi na Biashara Duniani..... 5
3.0.2. Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki............ 6
3.0.3. Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi Nyengine Duniani. ............................... 7
3.0.4. Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. ................................................ 8
3.0.5. Hali ya Chakula na Bei Katika Soko la Zanzibar ............................................. 9
**4.0. MWENENDO WA VIWANDA ..................11**
**5.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 ......................14**
5.0.1. Ukusanyaji wa Mapato........................ 14
5.0.2. Mafanikio ya Wizara............................ 15
5.0.3. Changamoto za Wizara........................ 16
**6.0. MATUMIZI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024...........17**
**7.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024................................................18**

PR0101: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. ....................................18
SR010101: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji ................................19
SR010102: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ................................................21
SR010103: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. .......................................24
PR0102: Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali .................................25
SR010201: Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda ...........................................26
SR010202: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali .............................28
PR0103: Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara.......................................31
SR010301: Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji .......................32
SR010302: Programu Ndogo ya Uwezeshaji Biashara ................................34
SR010303: Programu Ndogo ya Utengamano wa Kibiashara ..........................42
**8.0.MASHIRIKIANO NA TANTRADE .............. 43**
**9.0.UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 – MACHI, 2024.................................. 44**

9.0.1. Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Parks) .................. 45
9.0.2. Mradi wa Kuyaendeleza Maeneo ya Maonesho ya Biashara Dimani. .......................... 47
9.0.3. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar. ............................................ 48
9.0.4. Programu ya Kuimarisha Wajasiriamali kupitia Huduma za Maendeleo ya Biashara (BDS) na Kuboresha Ubora na Uzalishaji (KAIZEN) ............................................ 49
**10.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI AMBAZO HAZIPOKEI RUZUKU SERIKALINI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023- MACHI 2024. 51**
10.0.1. Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ...... 51
10.0.2. Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) ................................ 54
10.0.3. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ...... 56
10.0.4. Kampuni ya Mwani Zanzbar ( ZASCO) . 59
**11.0. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ........................................61**
11.0.1. Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2024/2025 ...................................... 61
Sekta ya Viwanda ............................................ 62
Kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko ........ 63
Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma ............................................... 64
Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) . 66

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS).................... 66
Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ................... 67
Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) .............. 68

**12.0.MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025 ........................................68**

**13.0.MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............72**

13.0.1.Mapato ya Serikali ................................ 72
13.0.2.Matumizi ............................................... 73

**14.0.HITIMISHO ..........................................75**

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

## MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN,

## KATIKA BARAZA LA WAWAKILI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## 1.0. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Awali kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kuweza kukutana hapa leo katika Baraza hili lako Tukufu tukiwa tunaendelea kushughulikia majukumu ya Kitaifa katika hali ya amani na utulivu. Namuomba Mola wetu Mtukufu azidi kutupa neema na uwezo wa kuendelea na ujenzi wa Taifa letu na watu wake.

2. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, naomba kutumia nafasi hii kupitia Baraza lako Tukufu, kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada na kasi za kuiletea maendeleo Zanzibar

zinazoonekana kwa uwazi na ambazo zimeleta maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii pamoja na kuendeleza amani na utulivu nchini. Aidha, namshukuru kwa kuendelea kuniamini kwa kunipa dhamana ya kusimamia maendeleo ya sekta za Biashara na Viwanda katika nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa mashirikiano na ushauri wake anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Hakika ushauri anaonipatia umenisaidia sana katika kuleta kasi ya maendeleo ya sekta ya Biashara na Viwanda Zanzibar. Aidha, napenda kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Nawapongeza Viongozi hao kwa kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake.

4. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nitumie fursa hii ya pekee kutoa shukrani maalum kwa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inayoongozwa na Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini pamoja na Wajumbe

wake wote kwa kuyachambua mapendekezo ya awali ya bajeti hii ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na kuweza kuridhia kwa kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa kwa Mapato na Matumizi ya mwaka 2024/2025. Wizara itaendelea kuzingatia na kutekeleza maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwa ajili ya utekelezaji wake.

5. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa dhati wewe binafsi kwa kuliongoza vizuri Baraza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kusimamia vyema mijadala inayoendeshwa katika Baraza hili.

6. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, nawapongeza Wafanyabiashara, Wawekezaji katika Viwanda na Wazalishaji mbali mbali kwa kuunga mkono juhudi za Serikali za kutokupandisha bei za vyakula hususani katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kuwawezesha wananchi kupata unafuu wa bei za vyakula wakati wa kutekeleza ibada ya funga.

7. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukrani na maelezo hayo ya awali, naomba kuanza Hotuba hii kwa kuwasilisha utekelezaji wa malengo

ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 na hatimae kuwasilisha mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## 2.0. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA.

**8. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imeundwa na Idara nne (4) ambazo ni Uendeshaji na Utumishi, Mipango, Sera na Utafiti, Maendeleo ya Viwanda, Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na Afisi Kuu Pemba. Aidha, inasimamia Taasisi 11 ambazo ni ZFCC, ZFCT, ZAWEMA, ZNBC, SMIDA, BLRC, COSOZA, ZBS, ZSTC, BPRA na ZASCO na inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:-

i. Kuandaa na kusimamia Mipango, Sera, Sheria na Tafiti zinazohusiana na sekta zilizo chini ya Wizara;
ii. Kusimamia kuwepo kwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji;
iii. Kusimamia na kuimarisha mazingira mazuri ya ufanyaji Biashara;
iv. Kuhakikisha bidhaa na huduma zinazozalishwa zinakidhi viwango vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
v. Kuhakikisha uwepo wa masoko kwa bidhaa za ndani katika masoko ya Nje ya nchi;

vi. Kusimamia na kukuza maendeleo ya Viwanda;
vii. Kusimamia shughuli za usajili wa biashara na mali;
viii. Kusimamia usawa wa Vipimo katika ushindani wa kibiashara;
ix. Kusimamia utoaji wa leseni ili kupunguza urasimu na kurahisisha utoaji wa leseni na vibali;
x. Kukuza mahusiano kati ya Sekta Binafsi na Serikali; na
xi. Kusajili, kukusanya na kugawa mirabaha kwa wamiliki husika wa haki miliki waliosajiliwa.

## 3.0. MWENENDO WA BIASHARA

### 3.0.1. Hali ya Uchumi na Biashara Duniani.

9. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Ripoti ya Biashara pamoja na Takwimu Duniani (Global Trade Outlook and Statistics April, 2024) Mwenendo wa biashara Duniani kwa kipindi cha mwaka 2023 umeshuka kwa asilimia 1.2 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo ukuaji wa biashara ulifikia asilimia 3.0. Kupungua huko kumetokana na kasi ya bei ya nishati na mfumko wa bei uliotokana na mahitaji makubwa ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

10. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2023 usafirishaji duniani umeshuka kwa asilimia 5.0 na kufikia Dola za Kimarekani trilioni 24.01. Hali hii imetokana na kushuka kwa usafirishaji kwa nchi za Shirikisho la Urusi kwa asilimia 28, kupungua kwa uzalishaji viwandani kwa Bara la Asia ikiwemo China (-5%), Japani (-4%), Jamhuri ya Watu wa Korea ya Kusini (-8%) na Marekani (-2%). Aidha, hali ya uagiziaji biashara Duniani kwa mwaka 2023 hususani katika Bara la Ulaya imeshuka ikilinganishwa na mwaka 2022. Hali hii ilisababishwa na kuongezeka kwa bei za nishati ya mafuta na gesi katika Bara la Ulaya.

### 3.0.2. Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

11. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023, Zanzibar imesafirisha bidhaa katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zenye thamani ya Shilingi milioni 9,932.2 sawa na asilimia 9.1 ya usafirishaji wote. Nchi ya Kenya ndio iliyofanya biashara kubwa na Zanzibar ambapo bidhaa za vitenge na khanga zilisafirishwa.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023, Zanzibar imeagiza bidhaa kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zenye thamani ya Shilingi

milioni 4,080.1 sawa na asilimia 0.3 ya uagiziaji wote. Nchi ya Kenya ndio iliyofanya biashara kubwa na Zanzibar ambapo bidhaa za saruji ziliagizwa kutoka nchi hiyo.

### 3.0.3. Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi Nyengine Duniani.

**13. Mheshimiwa Spika,** Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji wa bidhaa nje umepelekea hali ya biashara kwa ujumla kuimarika, ambapo kwa mwaka 2023 Zanzibar ilifanya biashara yenye thamani ya Shilingi bilioni 1,611 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1,439 kwa mwaka 2022 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 12. Bidhaa zilizosafirishwa kwenda nje ya Nchi ni pamoja na karafuu, vitenge, khanga, mwani, mazao ya baharini, vyuma chakavu, makapi ya ngano na ngozi za n'gombe na bidhaa zilizoagizwa ni bidhaa za chakula pamoja na vipuri vya magari.

**14. Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 109.26. Kiwango hicho cha usafirishaji ni sawa na punguzo la asilimia 39 ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 180.37 uliofanyika kipindi cha mwaka 2022. Hii imetokana na usafirishaji mdogo

wa karafuu. Bidhaa hizo zilisafirishwa katika masoko ya Singapore, Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Indonesia, India na Denmark.

**15. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1,501 kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na uagiziaji wa Shilingi bilioni 1,258 kwa mwaka 2022. Bidhaa ambazo Zanzibar imeagiza kutoka nchi za nje ni pamoja na mafuta, bidhaa za Viwandani, vyombo vya usafiri, nguo na bidhaa za chakula. Aidha, Zanzibar imeagiza bidhaa kwa wingi kutoka nchi za Falme za Kiarabu, China, India, Pakistani, Brazil, Uturuki, na Vietnam.

### 3.0.4. Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.

**16. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa usafirishaji Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kipindi cha mwaka 2023, Zanzibar ilisafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara zenye thamani ya Shilingi bilioni 157.94 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 37.64 zilizosafirishwa mwaka 2022. Miongoni mwa bidhaa zilizosafirishwa kwenda Tanzania Bara ni pamoja na chuma chakavu, mafuta ya kupikia, mchele wa basmati na bidhaa nyengine za vyakula vya makopo. Aidha, katika kipindi cha

mwaka 2023, Zanzibar iliagizia kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 431.54 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 375.80 kwa mwaka 2022.

### 3.0.5. Hali ya Chakula na Bei Katika Soko la Zanzibar

17. **Mheshimiwa Spika,** Hali ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula hapa Nchini inaendelea kuridhisha na vyakula vyote muhimu vinaendelea kupatikana bila ya usumbufu. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya Tani 80,843 za Mchele, Tani 15,067 za Sukari, Tani 1,643 za Unga wa ngano na Tani 96,750 za Mafuta ya kula ziliingizwa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani. Bidhaa hizo zinatoka katika Nchi za India, Brazil, Uturuki, Pakistani, na Vietnam. Hata hivyo, uzalishaji wa ndani uliendelea kwa bidhaa za unga wa ngano ambao unazalishwa na kiwanda cha Zanzibar Milling kilichopo Mtoni. Takwimu zinaonesha jumla ya Tani 38,482 za unga wa ngano na Tani 4,560 za Sukari zilizalishwa nchini kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Mchanganuo unaonekana katika **Kiambatanisho Nambari 1**.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa bei za bidhaa muhimu kama vile mchele, unga wa ngano pamoja na sukari katika soko la ndani zimekuwa zikiongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hizo katika masoko ya dunia na kuongezeka kwa thamani ya fedha ya Kimarekani dhidi ya Fedha ya Tanzania pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji. Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda iliendelea na utaratibu wa kupanga bei elekezi kwa bidhaa muhimu za chakula kama vile Mchele, Sukari, Mafuta ya kupikia na Unga wa Ngano pamoja na kusimamia bei hizo kwa lengo la kuleta unafuu wa bei kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa kipindi cha Mwezi mtukufu wa Ramadhani, Serikali ilisamehe kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa bidhaa ya sukari kwa lengo la kupunguza bei kwa bidhaa hiyo kwa Wananchi. Kufuatia upangaji huo wa bei, Wizara ilishirikiana na makundi mbali mbali ikiwemo Wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa nchini, Mamlaka za kodi, Taasisi zinazotoa tozo kwa wafanyabiashara. Bei za bidhaa hizo muhimu zinaonekana katika **kiambatanisho Nambari 2.**

## 4.0. MWENENDO WA VIWANDA

19. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023 mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa (GDP) uliongezeka kufikia asilimia 20 kutoka asilimia 19.4 kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo linatokana na uanzishwaji wa viwanda vipya kama vile kiwanda cha kuzalisha matangi ya maji kilichopo Nyamanzi na kiwanda cha vifaa vya umeme ( Africab) kilichopo mtaa wa Viwanda Amani.

20. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha kuzalisha matenki ya maji Aishan Coy Ltd. Kilichopo Nyamanzi kimeanza uzalishaji mwaka wa fedha 2023/2024. Uwezo wa uzalishaji wa kiwanda hicho kwa siku ni matenki saba 7 ya ujazo tofauti. Kwa sasa bidhaa za kiwanda hicho zinapatikana kwa wingi katika soko la Zanzibar, kiwanda hicho kinategemea kutoa nafasi 30 za ajira. Kwa upande wa kiwanda kiwanda cha Africab kinachozalisha Nyaya za umeme katika eneo tengefu la viwanda Amani kinaendelea na uzalishaji wa nyaya za umeme za aina mbali mbali. Kiwanda hiki kimeanza uzalishaji mwaka 2022.

21. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation (ZMCL) kimeongeza uwezo

wa kuzalisha kutoka tani 64,800 hadi kufikia tani 119,880 za unga wa ngano. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya tani 49,355.38 za unga wa ngano zimezalishwa sawa na asilimia 41.17 ya uwezo wa Kiwanda. Aidha, Kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 200, ambapo Wafanyakazi 137 ni wa kudumu na 63 ni wa muda.

**22. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha nguo cha Basra Textile Mills Limited kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kimeweza kuzalisha mita 1,723,185.33 za Vitenge na mita 404,203.97 za Khanga ambapo Vitenge na Khanga hizo zimeweza kuingia katika masoko ya nchi za Afrika Mashariki (EAC) na soko la Kusini mwa Afrika (SADC). Kiwanda hicho kwa sasa kimeweza kuajiri jumla ya wafanyakazi 314.

**23. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha sukari Mahonda kimeweza kuzalisha tani 8,760 za sukari kwa mwaka 2023/2024 ukilinganisha na tani 4,242 kwa mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 206.

**24. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Drop of Zanzibar kimeweza kuzalisha lita 37,528,441.65 za maji kwa mwaka 2023/2024 ukilinganisha na lita 35,741,373 za maji kwa mwaka 2022/2023 ongezeko hili na sawa na asilimia 105.

**25. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha chumvi (Swahili salt) kilichopo Wawi Chake-Chake Pemba kimeanza uzalishaji mwaka 2013. Uwezo wa uzalishaji wa kiwanda hicho ni tani elfu tatu (3000) za chumvi kwa mwaka.

**26. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zanto kilichopo Shakani kinajishughulisha na kuchakata mazao na kwa sasa kimeanza na uchakataji wa zao la tungule kwa ajili ya kutengeneza "tomato sauce " pamoja na majani ya chai. Uwezo wa kiwanda hicho kwa upande uzalishaji wa 'tomato sauce' ni lita thelathini na mbili elfu (32,000) kwa siku.

**27. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Viwanda vikubwa vilivyotajwa hapo juu, Wizara inathamini juhudi zinazofanywa na viwanda vyengine vidogo vyenye kuzalisha bidhaa za aina mbali mbali kama vile maji, samani, vifungashio, chakula cha kuku, chumvi na uchakataji wa matunda.

**28. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda imeendelea kuimarisha eneo la mtaa wa viwanda (industrial park) liliopo Dunga na hadi nawasilisha makadirio ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2024/2025 ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 65 na mradi wa maji umefikia asilimia 45.

Aidha, napenda kuliarifu Baraza lako kwamba Wizara inaendelea na mazungumzo na kampuni ya AFRICA BIO CHEM PHARMA ya China ambayo inakusudia kujenga kiwanda kikubwa cha dawa za magonjwa ya binaadamu katika ukanda wa Afrika mashariki. Mazungumzo yanaendelea vizuri na hivi karibuni Wizara itasaini mkataba na kampuni hiyo ili mradi huo uanze.

## 5.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

### 5.0.1. Ukusanyaji wa Mapato

**29.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 1.75** kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi bilioni 1.30**. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **Shilingi bilioni 1.10** zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya makusanyo.

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Mnamo Julai 2023 majukumu ya Afisi ya Hakimiliki (COSOZA)

yalihamishiwa rasmi Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, ambapo kupitia Taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi milioni 150. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 COSOZA ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi milioni 130 kutoka katika kifungu cha Mirabaha. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya Shilingi milioni 135 zilikusanywa sawa na asilimia 105 ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi cha miezi tisa (9). Mchanganuo wa mapato kwa ujumla unaonekana katika **kiambatanisho nambari 3.**

### 5.0.2. Mafanikio ya Wizara

**31. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa ni kukamilisha kwa asilimia 80 ya ujenzi wa eneo la maonesho ya kibiashara Dimani, kukamilika kwa Mpango Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre), kukamilika kwa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 7.83 kwa kiwango cha kifusi pamoja na kuanza ujenzi wa miundo mbinu ya maji na tangi lenye ujazo wa lita milioni moja katika eneo la viwanda Dunga. Aidha, Wizara imejenga vituo vitatu (3) Jumuishi vya Urasimishaji Biashara Unguja

na Pemba kwa lengo la kuimarisha huduma za usajili wa biashara . Vile vile, imekamilisha ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu zao la mwani katika eneo la Chamanangwe Pemba ambacho kitasarifu mwani aina ya "Spinosum" na "Cottonii" pamoja na kuongezeka kwa Maabara mpya nne na kituo cha kisasa cha ukaguzi wa vyombo vya moto.

### 5.0.3. Changamoto za Wizara

**32. Mheshimiwa Spika,** Changamoto zinazoikabili Wizara ni pamoja na :-

i. Mazingira yasiyo rafiki kwa Wafanyakazi kwa baadhi ya Taasisi ambazo zinatumia majengo ya zamani ya Mji Mkongwe.
ii. Kutokuwepo kwa mfumo maalumu wa utoaji taarifa kwa Taasisi zote zinazohusiana na Miungano ya Makampuni na masuala ya Ushindani na kumlinda mtumiaji.
iii. Uingiaji mdogo wa fedha za matumizi mengineyo unaopelekea kutokutimiza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.
iv. Uhaba wa rasilimali watu na vyombo vya usafiri katika kutekeleza majukumu ya Wizara na Taasisi zake.
v. Uharamia wa kazi za hakimiliki na ugumu wa kufanya malipo ya mirabaha kwa watumiaji wa kazi za Haki miliki.

## 6.0. MATUMIZI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi bilioni 37.41 kwa ajili ya kutekeleza programu zake. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 Wizara ilipanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 34.75, ambapo jumla ya Shilingi bilioni 19.45 sawa na asilimia 56 ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana. Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha miezi tisa ni sawa na asilimia 52 ya makisio ya mwaka. Kati ya fedha hizo jumla ya Shilingi bilioni 4.20 ziliingizwa kwa ajili ya mishahara, Shilingi bilioni 13.76 kwa ajili ya kazi za maendeleo na Shilingi bilioni 1.49 kwa kazi za kawaida. Mchanganuo wa matumizi hayo unaonekana katika **kiambatisho Nambari 4.**

34. **Mheshimiwa Spika,** Kuongezeka kwa bajeti hiyo kumetokana na maamuzi ya Serikali ya kuirejesha SMIDA Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutoka Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji mnamo Novemba, 2023, sambamba na kuhamishia majukumu ya Afisi ya Hakimiliki (COSOZA) kutoka Wizara ya Habari, Vijana na Utamaduni kuja Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Julai 2023.

## 7.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Programu kuu tatu ambazo ni Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali na Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara. Programu hizo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara za Wizara, Afisi Kuu Pemba pamoja na Taasisi zake ikiwemo ZFCC, BLRC, ZNBC, ZFCT, COSOZA, SMIDA na ZAWEMA, ambapo utekelezaji wa programu hizo ni kama ifuatavyo: -

**PR0101: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.**

36. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kutoa huduma za Kiofisi kwa ufanisi na ustawi wa sekta ya Biashara na Viwanda. Programu hii imegawika katika Programu Ndogo tatu (3) kama ifuatavyo:-

i. Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara.

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.

iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 4.05** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024, Programu hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 3.00** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi bilioni 2.32** zimeingizwa sawa na asilimia 77 kwa ajili ya kutekeleza programu hii. Utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:-

**SR010101: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina jukumu la kusimamia rasilimali watu, ununuzi wa vifaa vya Ofisi na kuratibu mikutano ya majadiliano ya biashara na viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

i. Vikao saba (7) vya Bodi ya Zabuni vimefanyika ambavyo vilijadili Mpango wa Manunuzi wa Wizara kwa mwaka 2023/2024, Mpango Mkuu

wa eneo la Maonyesho Dimani na Mpango wa Ununuzi wa Samani za Wakala wa Mizani na Vipimo;

ii. Imewapatia Wafanyakazi watatu (3) (mwanamke 1 na wanaume 2) mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Ukatibu Muhtasi, Hesabu na Fedha na Uongozi wa Rasilimali Watu. Aidha, Wafanyakazi wanne (4) (wanawake 2 na wanaume 2) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Uhusiano wa Umma na Mawasiliano na Utunzaji kumbukumbu. Jumla ya Wafanyakazi watano (5) wanaendelea na masomo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika ngazi na kada tofauti;

iii. Wafanyakazi 32 (wanaume 18 na wanawake 14) wamepatiwa likizo la kawaida, Wafanyakazi 13 wamepatiwa likizo la dharura na wawili (2) likizo ya uzazi;

iv. Huduma mbali mbali za Ofisi zimetolewa zikiwemo, huduma za kimtandao, ulipaji wa kodi ya jengo la Ofisi, upatikanaji wa maji, matengenezo ya Ofisi pamoja na huduma za umeme ; na

v. Wizara imeratibu ushiriki wa Viongozi katika Mikutano, Semina na Makongamano ya Kitaifa,

Kikanda na Kimataifa inayohusu Kongamano la pili la AfCFTA la Wanawake katika Biashara, Mkutano wa jukwaa la Biashara Mtandao kwa Afrika Mashariki nchini Nairobi, Mkutano wa Kitaifa wa ufuatiliaji vikwazo vya Biashara visivyo vya kodi na Mkutano wa jukwaa la mifumo ya chakula Afrika.

**39. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Ofisi ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.58** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024 Programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 1.86**. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **Shilingi bilioni 1.41** sawa na asilimia 75 zimeingizwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

**SR010102: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara**

**40. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kutoa huduma za uandaaji na uibuaji wa tafiti, uandaaji na utekelezaji wa Mipango pamoja na usimamizi wa takwimu za Wizara. Utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imekamilisha mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara kwa mwaka 2024/25 – 27/28. Mapitio hayo yamelenga kuweka mazingira mazuri ya biashara, kuongeza thamani kwa bidhaa ya Mwani na Karafuu pamoja na kuongeza usafirishaji;

ii. Wizara imefanya tathmini ya mazingira ya biashara Zanzibar kwa kufanya mapitio ya Sera na Sheria zinazohusiana na masuala ya Biashara na Viwanda. Tathmini hiyo imelenga kutatua vikwazo na changamoto za ufanyaji biashara nchini;

iii. Kukamilika kwa Utafiti wa Nakisi ya Biashara ambao umeangalia sababu za urari wa biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara;

iv. Wizara imeandaa taarifa mbali mbali za robo na nusu mwaka kwa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo, taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha Miaka mitatu (3), taarifa ya Miradi na uandaaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Viwanda ya Zanzibar ya 2019 na Sera ya Wajasirimali ya 2020;

v. Kukamilika kwa Mpango Mkuu (Master Plan) wa Ujenzi wa Uwanja wa Maonesho wa Kimataifa Dimani;

vi. Kukamilika kwa uandaaji wa Dhana za Awali za miradi sita na tafiti sita zinazolenga ukuzaji wa biashara na uendelezaji wa Viwanda;

vii. Wizara imeandaa taarifa za takwimu za robo na nusu mwaka zinazohusiana na Biashara na Viwanda na kuziwasilisha Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali; na

viii. Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Mipango wa Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya juu ya uandaaaji wa Mpango wa matumizi ya Muda wa Kati 2024/25-2026/27, vipaumbele, uingizaji wa bajeti pamoja na uandaaji wa bajeti inayozingatia jinsia ambapo jumla ya Mafisa 20 walipatiwa mafunzo hayo.

41. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 570.49** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024 Programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi milioni 446.89** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi milioni 286.18** sawa na asilimia 64 zimeingiziwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010103: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.**

**42. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

i. Wizara imeratibu ushiriki wa Wajasiriamali katika maonesho ya Sabasaba, maonesho ya siku ya Chakula Duniani na Tamasha la 10 la Biashara. Aidha, jumla ya vikundi 19 vilishiriki maonesho hayo;

ii. Vikundi vinane (8) vimepatiwa mafunzo ya utengenezaji na usarifu wa bidhaa kwa kutumia zao la mwani. Mafunzo hayo yalilenga utengenezaji wa bidhaa za Sabuni, Losheni, Mafuta ya nywele, Mafuta ya kujipaka, Juisi na Jamu;

iii. Jumla ya Viwanda sita (6) vimepatiwa mafunzo ya uendeshaji shughuli za uzalishaji kwa mujibu wa Sheria ya Viwanda, kati ya hivyo viwanda vitatu (3) vinatoka Wilaya ya Chake Chake na vitatu (3) vinatoka Wilaya ya Wete;

iv. Mikutano mitatu (3) ya kusikiliza changamoto za Wajasiriamali na kuweza kuzitatua katika Wilaya zote za Pemba imefanyika pamoja na kuvitembelea Vikundi 42 vya Wajasiriamali;

v. Vikao vitatu (3) kwa Wafanyabiashara juu ya kuzuia ongezeko la bei elekezi kwa bidhaa muhimu za Mchele, Sukari na Unga wa Ngano vimefanyika; na

vi. Wizara imewapatia likizo Wafanyakazi 12 (wanawake 7 na wanaume 5) kati ya hao wafanyakazi wanane (8) wamelipwa stahiki zao.

**43. Mheshimiwa Spika,** Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 907.38** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 programu hii ilipangiwa **Shilingi milioni 693.19**. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi milioni 633.95** sawa na asilimia 91 zimeingiziwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

## PR0102: Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

**44. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali inatekelezwa na

Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA). Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji wa Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Programu hii ina jukumu la kuongeza mchango wa sekta ya uzalishaji Viwandani katika Pato la Taifa.

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 27.29** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024, Programu hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 26.47** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi bilioni 6.72** zimeingizwa sawa na asilimia 25 kwa ajili ya kutekeleza programu hii. Utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:-

**SR010201: Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda**

46. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kutoa huduma ya kuimarisha sekta ya viwanda. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya BRELA imefanya vikao vya wadau wa Viwanda na

kuipitia Sheria ya Taifa ya Viwanda ya mwaka 1967 kwa lengo la kuimarisha Sheria hiyo ili iweze kukidhi mahitaji yaliyopo sasa. Kwa sasa Wizara itaweza kutoa leseni za Viwanda kwa upande wa Zanzibar kwa kutumia Sheria hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 13 ya nyongeza ya kwanza ya mambo ya Muungano.

ii. Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao imeandaa Mfumo wa Takwimu za Viwanda (Industrial Registration Database) kwa ajili ya kupokea taarifa za viwandani (progress report) na Mfumo huo unatarajiwa kuanza kutumika kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

iii. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Tanzania Bara imetoa mafunzo kwa watendaji 21 kwa Taasisi za Serikali yanayohusiana na ufanisi wa uzalishaji Viwandani. Aidha, Viwanda vitatu (3) vimepatiwa mafunzo ya mpangilio mzuri wa uendeshaji shughuli za uzalishaji viwandani kivitendo ambapo viwanda vitatu vimepatiwa vyeti vya kukamilisha mafunzo hayo akiwemo ZANTO Company, LOTAH Group of Company na INAYA Company.

iv. Wizara imefanya ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara katika eneo la viwanda Dunga ili kuhakikisha utekelezaji wa ujenzi huo unaenda sambamba kwa mujibu wa Mkataba uliopo.

**47. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 26.39** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 25.74** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi bilioni 6.53** sawa na asilimia 25 ya fedha zilizopangwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 6.01** ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo na **Shilingi milioni 528.25** kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara.

**SR010202: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali**

**48. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya maendeleo ya Wajasiriamali inatekelezwa na Idara ya Viwanda na Wakala wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) na ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera ya MSME's na Uendelezaji wa Wajasiriamali na kuongeza mchango wa uzalishaji wa sekta ya wajasiriamali katika pato la Taifa. Utekelezaji wa

Programu hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

i. Wizara imevitembelea na kuvikagua Viwanda 65 na kuzifanyia matengenezo mashine nne (4) za Viwanda hivyo. Aidha, Wajasiriamali 17 (wanawake 11 na wanaume 6) wenye Viwanda wamesaidiwa katika ushiriki wa Maonesho ya Sabasaba;

ii. Wizara imeratibu mashindano ya Ubunifu katika Tamasha la 10 la Maonesho ya Biashara ambapo Bunifu sita (6) za Mashine na mifumo yenye tija kwa Taifa imebuniwa. Ubunifu huo ni pamoja na ubunifu wa kuvuna umeme wa jua; ubunifu wa kuangalia kiwango cha maji katika tangi; ubunifu wa kupima udongo; ubunifu wa kusoma mtandaoni kiurahisi; ubunifu mfumo wa mpangilio wa Magari ; na ubunifu wa kutunza mazingira;

iii. Wizara imetoa mafunzo kwa Wajasiriamali wenye viwanda na wajasiriamali wazalishaji (30) (wanawake 18 na wanaume 12) juu ya utumiaji wa mfumo wa kielektroniki katika kuuza bidhaa zao ikiwa ni kipengele cha ukamilishaji wa Jukwaa la Masoko Mtandaoni; na

iv. Wazalishaji wenye viwanda 85 wamepatiwa mafunzo kati yao (25) (wanawake 20 na wanaume 5) wamepatiwa mafunzo ya utaalamu wa uzalishaji na ubora; Wazalishaji (30) (wanawake 5 wanaume 25) wamepatiwa mafunzo ya namna bora na salama kwa uzalishaji chumvi viwandani. Aidha, Wazalishaji 30 kutoka katika vikundi vitano (5) wamepatiwa mafunzo ya utengenezaji Sabuni za miche ili kufikia uzalishaji wa mazao ya kimkakati katika Mikoa yetu.

**49. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 897.42** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo **Shilingi milioni 11.32** ni kwa ajili ya kutekeleza huduma ya Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's kwa upande wa Idara ya Viwanda na **Shilingi millioni 886.10** kwa SMIDA . Kwa kipindi cha miezi tisa (9) jumla ya **shilingi milioni 730.85** zimepangwa. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **Shilingi milioni 182.11** zimeingizwa sawa na asilimia 25 kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

## PR0103: Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara

**50. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Programu hii ina Programu ndogo tatu ambazo ni :-

i. Programu ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji.
ii. Programu ya Uwezeshaji Biashara.
iii. Programu ya Utengamano wa Kibiashara.

**51. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 6.06** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024, Programu hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 5.26** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi bilioni 10.40** zimeingizwa sawa na asilimia 197 kwa ajili ya kutekeleza programu hii. Kuongezeka kwa matumizi hayo kumetokana na mabadiliko ya nyongeza mpya ya mishahara kwa Taasisi zilizopo chini ya Wizara yalifanyika kuanzia Agosti, 2023 sambamba na uhaulishaji wa vifungu vya mradi wa Maeneo tengefu ya Viwanda kutumika katika Mradi wa Kuyaendeleza Maeneo ya Maonesho ya Biashara Dimani. Utekelezaji shughuli zilizopangwa

katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:-

**SR010301: Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji**

**52. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko ina jukumu la kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika usafirishaji wa bidhaa katika masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa pamoja na kuongeza fursa za masoko. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imetekeleza shughuli kama ifuatavyo:-

i. Wizara imeratibu na kuandaa Tamasha la kumi (10) la Biashara la mwaka 2024, ambalo hufanyika kila mwaka ifikapo Januari ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka 2024 jumla ya washiriki 376, kati ya hao Taasisi za Serikali 134, Kampuni 43, Wafanyabiashara na Wajasiriamali 199 walishiriki. Aidha, Wajasiriamali tisa (9) kutoka nje ya nchi walishiriki, kati ya hao, wanne (4) ni kutoka Uganda, Wawili (2) Burundi na watatu (3) kutoka Kenya, Rwanda na Zambia;

ii. Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Holiday Market Festival iliandaa Maonesho ya Kibiashara na Utalii yaliyofanyika katika viwanja vya Maisara Septemba, 2023 ambapo jumla ya washiriki sitini (60) kutoka ndani na nje ya Zanzibar walishiriki;

iii. Wizara imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) ambapo jumla ya washiriki 50 kutoka Zanzibar walishiriki. Kati ya hao, Wajasiriamali 34, Taasisi za Serikali na Kampuni Binafsi 16 zimeshiriki;

iv. Wizara imeratibu ushiriki wa Wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonesho ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaliyofanyika Disemba 2023 nchini Bujumbura ambapo jumla ya Wajasiriamali 26 ( wanaume 9 na 17 wanawake) wameshiriki; na

v. Wizara imekamilisha mapitio ya Kanuni tano (5) zinazohusiana na biashara kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa masuala ya biashara ya bidhaa na huduma nchini. Kanuni hizo ni Kanuni ya Bidhaa Zinazodhibitiwa; Kanuni ya Mauziano kwa Njia ya Mkopo; Kanuni ya Biashara ya Chuma Chakavu; Kanuni ya Usimamizi

na Uendeshaji wa Maonesho na Kanuni ya Ufanyaji Biashara.

53. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 3.81** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 3.43** hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **Shilingi bilioni 9.26** sawa na asilimia 270 ziliingizwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 7.75** ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo na **Shilingi bilioni 1.51** zimeingizwa kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara.

**SR010302: Programu Ndogo ya Uwezeshaji Biashara**

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ambazo zina jukumu la kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

i. Kufanyika kwa ukaguzi katika maeneo ya uingizaji na usafirishaji bidhaa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi kwa Wafanyabiashara ambapo kupitia ukaguzi huo, Wafanyabiashara 156 wamepatiwa hati za usajili wa biashara (Import /Export Registration Certificate);

ii. Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imefanya mafunzo ya urasimishaji wa Biashara kwa wafanyabiashara 200 (Wanawake 126 na Wanaume 74) katika Wilaya ya Chake Chake Pemba kwa lengo la kuwahamasisha wafanyabiashara kufanya biashara zao kwa kutumia mifumo iliyo rasmi;

iii. Kukamilika kwa mapitio ya leseni, vibali na ruhusa za ufanyaji Biashara Kisekta ambapo jumla ya Sekta 14 zimepitiwa, mapitio ya Tozo 250 na Kanuni 55 kwa Mamlaka za utoaji leseni, vibali na ruhusa za ufanyaji Biashara pamoja na kuwasilisha ripoti za mapitio hayo Serikalini;

iv. Kufanyika kwa ukaguzi wa Mamlaka 44 za utoaji leseni kwa kuangalia utekelezaji wa miongozo inayotolewa na Baraza la Leseni katika kuondosha urasimu wa ufanyaji Biashara Zanzibar. Katika ukaguzi huo, Baraza la Usimamizi wa Leseni limegundua kukosekana kwa baadhi ya Kanuni na Miongozo katika Mamlaka na uwezo mdogo wa kifedha ambao unasababisha kuchelewa kwa uanzishwaji wa mifumo ya kielektroniki;

v. Uhakiki wa mita 85 za vituo vya Mafuta, tisa (9) za Uwanja wa Ndege, Mizani za Maduka 600,

Magari 11 ya kusambazia Mafuta, Matangi 56, Keni tano (5) za kupimia mafuta na bidhaa saba (7) za Viwandani zilizofungashwa;

vi. Wizara imefanya uhakiki wa ujazo wa mafuta katika Meli zinazotumika kuleta mafuta katika mfumo wa pamoja ambapo jumla ya lita 184,372,958 zimehakikiwa;

vii. Kukamilika kwa "Board Charter" na Kanuni za maadili za Baraza la Ushindani na zimeshaanza kutumika;

viii. Wizara imeshiriki Mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na ufunguzi wa Tawi la Mtandao la Wanawake wa Kiafrika wa ACFTA (AWNA) Tanzania, Mkutano wa Chama cha Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (TRAMP), Kikao cha pamoja baina ya ZFCT na FCT na Warsha ya ufunguzi wa utafiti wa masuala ya Miungano ya Kampuni;

ix. Wizara imetoa mafunzo kwa Masheha, Maafisa Waandamizi wa Mamlaka za Udhibiti, Wawekezaji na Wafanyabiasha wakubwa, Wajumbe wa Baraza la Biashara la Mikoa ya Mjini Magharibi, Kusini na Kaskazini Pemba pamoja na kuandaa makala na kurusha

hewani vipindi vya radio na televisheni juu ya uelewa wa majukumu ya Baraza la Ushindani Zanzibar;

x. Rasimu ya Kanuni ya Uchangiaji wa Fedha wa Baraza la Ushindani Halali wa Biashara imetayarishwa pamoja na kufanya mapitio ya Sheria ya Ushindani nambari 5 ya mwaka 2018;

xi. Wizara imesajili na kuzisimamia kazi za hakimiliki 425, Wabunifu wapya 58 na imetoa uthibitisho wa usajili husika wa kazi ya hakimiliki kwa Wabunifu hao.

xii. Wizara imewafikia Wasanii na Wabunifu Wakongwe 20 katika maeneo yao na kuwapatia kiasi cha fedha kinachotokana na eneo maalumu la mirabaha;

xiii. Wizara imefanya ukaguzi wa maeneo 253 ya watumiaji wa Hakimiliki ili kupunguza uharamia wa Hakimiliki na kuangalia matumizi sahihi ya kazi za hakimiliki kibiashara na kutoa leseni za Hakimiliki;

xiv. Wizara imepokea malalamiko matatu (3) juu ya uvunjwaji wa hakimiliki na tayari migogoro hiyo imeshapatiwa ufumbuzi na wamiliki wa hakimiliki hao wamelipwa haki zao;

xv. Wizara imeandaa Rasimu ya Sera ya Milki Bunifu Zanzibar kwa lengo la kukabiliana na maendeleo ya tasnia hii ya Milki Bunifu Kibiashara;

xvi. Katika jukumu la kutoa elimu juu ya masuala ya hakimiliki kwa wadau mbali mbali, Wizara kupitia Afisi yake ya COSOZA imeandaa na kurusha hewani vipindi 25 vya Redio na Televisheni. Vipindi hivyo vimetoa hamasa kwa Wabunifu, Wasanii na jamii kwa ujumla juu ya usimamizi wa hakimiliki na matumizi halali ya kazi za hakimiliki. Aidha, makala tatu (3) na vipeperushi juu ya masuala ya hakimiliki vimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau kupitia mitandao ya kijamii;

xvii. Wafanyakazi watano (5) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi yanayohusiana na uendeshaji wa mashtaka na mafunzo ya kugundua, kupunguza na kuzuia udanganyifu kwa Taasisi na mfanyakazi mmoja (1) amepatiwa mafunzo ya muda mrefu Shahada ya kwanza katika fani ya Maendeleo ya Mipango kupitia Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki;

xviii. Vikao vitatu (3) vya Kamati Tendaji ya Baraza la Biashara la Taifa vimefanyika kwa ajili ya kupitia utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Taifa la Biashara pamoja na maazimio ya

Jukwaa la Biashara. Sambamba na kupitisha agenda za Mkutano wa Sita wa Baraza la Taifa la Biashara na mikutano mitano (5) ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa yamefanyika;

xix. Vikao vinne (4) vya Kamati za Baraza la Taifa la Biashara vimefanyika kupitia taarifa za utekelezaji wa changamoto zilizowasilishwa na Wizara mbali mbali za kisekta ambapo changamoto hizo zilijikita katika masuala ya Kodi na matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki, usajili wa ardhi na mipaka ya maeneo ya uwekezaji, marejesho ya VAT, Gharama za alama ya ubora, changamoto za uwekezaji, michezo ya baharini na watembeza watalii wasiofuata kanuni na taratibu;

xx. Wizara imeshiriki Mikutano na Majukwaa tisa (9) ya Biashara ya ndani na nje ya Nchi, mikutano hiyo ni pamoja na Tamasha la Mapinduzi la Zanzibar; Maonyesho ya Biashara ya kitaifa (Zanzibar day); Mkutano wa kuandaa utekelezaji wa mradi wa kukuza masoko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya; Kongamano la Uwekezaji wa Biashara baina ya Tanzania na Asia; Kikao cha mazingira ya Biashara kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa maazimio ya TNBC; Mkutano wa Kamati ya Taifa ya Uwezeshaji

Biashara; na Semina maalum kuhusu Mpango wa Biashara wa Uingereza na nchi zinazoendelea;

xxi. Baraza la Biashara la Taifa limetoa mafunza ya muda mfupi kwa wafanyakazi sita (6) (wanawake 4 na wanaume 2) katika fani za mafunzo ya uhakiki, utunzaji kumbukumbu, Ukatibu Muhtasi, Uhasibu na Utawala;

xxii. Wizara imefanya ukaguzi wa Maduka 935, Maghala 82, Supermarket 45 kwa bidhaa za vyakula vya Makopo, bidhaa za matumizi ya Binaadamu pamoja na bidhaa zilizodhibitiwa kama vile Sukari, Unga wa Ngano na Mchele. Aidha, Wizara imebaini Wafanyabiashara 101 wa bidhaa ya Sukari wameuza kinyume na bei elekezi ambapo baadhi yao walipatiwa adhabu (faini) na baadhi yao kupewa elimu kwa mujibu wa Sheria;

xxiii. Wizara imepokea na kuyatolea maamuzi malalamiko ya Wafanyabiashara yanayohusiana na kughushi alama za biashara na kufanya udanganyifu na hadaa kwa watumiaji katika bidhaa wanazoziuza. Aidha, ufuatiliaji wa mwenendo wa bidhaa ya Saruji umefanyika kwa Waingizaji na Wasambazaji wa bidhaa hiyo;

xxiv. Wizara imebaini uwepo wa miungano ya makampuni baina ya ZK Venturer Ltd ya Zanzibar na LUX Collection ya Afrika ya Kusini ambayo haikutolewa taarifa rasmi kwa ZFCC, kupitia taarifa hiyo Wizara imewaandikia barua Makampuni hayo ya kuwataka kuwasilisha taarifa rasmi za miungano yao kwa mujibu wa sheria. Aidha, Wizara imewaandikia Barua Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) kuomba taarifa za wamiliki wa hisa za zamani na wa sasa ili kuweza kubaini kama kuna mabadiliko ya umiliki wa hisa katika kampuni hizo; na

xxv. Wizara imepitia na kukagua Mikataba 15 kwa lengo la kuondosha vigezo na masharti kandamizi kutoka katika Taasisi ya Mikopo ya Kifedha (Brac), Benki ya Azania na Benki ya NMB.

55. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.22** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2023 – Machi 2024 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 1.81** na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **Shilingi Bilioni 1.14** sawa na asilimia 63 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010303: Programu Ndogo ya Utengamano wa Kibiashara**

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha biashara huria ambayo itapelekea kuongezeka kwa masoko na uwekezaji baina ya Zanzibar na Nchi nyengine. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

**57. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika hatua ya kuimarisha Mashirikiano ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa imeweza kushiriki katika mikutano mbali mbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na masuala ya Biashara. Mikutano hiyo ni pamoja na Uondowaji wa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha, mkutano wa mapitio ya Sera ya Biashara kwa nchi masikini zinazoendelea Duniani, mkutano wa kongamano la Wanawake la Biashara chini ya mkataba wa Soko Huru la Afrika ili kuwajengea Wanawake uwezo wa kutumia fursa za Kibiashara katika soko hilo. Aidha, katika kuimarisha uhusiano wa kibiashara na Tanzania Bara, Wizara ilishiriki katika vikao vya uanzishwaji wa mfumo wa pamoja wa kielektroniki wa uondoshaji shehena maeneo ya forodha kwa ngazi ya wataalamu na Makatibu Wakuu. Mfumo huo una lengo la kukuza na kurahisisha ufanyaji Biashara Nchini.

**58. Mheshimiwa Spika,** Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 39.92** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2023 – Machi 2024 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi milioni 29.58** na hadi kufikia Machi 2024, programu ndogo hii imeingiziwa **shilingi milioni 1.57** kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

## 8.0. MASHIRIKIANO NA TANTRADE

**59. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Biashara na Viwanda na kuimarisha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa ndani ya Nchi, Wizara hufanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ili kuhakikisha biashara inakuwa nchini. Miongoni mwa maswala makuu ambayo Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imeshirikiana na TANTRADE kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ni pamoja na:-

i. Mashirikiano katika Uratibu wa maonesho mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yakiwemo Maonesho ya 47 ya Biashara ya Sabasaba ambapo kwa upande wa Zanzibar Taasisi mbalimbali za binafsi na Serikali pamoja na Wajasiriamali walishiriki katika maonesho hayo; Maonesho ya Viwanda,

maonesho ya 10 ya Kimataifa ya Biashara ya maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika Dimani na maadhimisho ya sherehe za Muungano yaliyofanyika Dimani.

ii. Wizara imeshirikiana na TANTRADE katika kuwapatia taarifa na taratibu za usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa nchini kupitia mfumo wa Trade Portal. Baadhi ya taarifa katika mfumo huo tayari zimeshaingizwa zikiwemo bidhaa za mchele, sukari, bidhaa za viungo, asali, dawa, mwani, karafuu na bidhaa nyengine. Taarifa zilizoingizwa kwenye mfumo huo zinaonesha taratibu za kufuata wakati wa uagizaji na usafirishaji bidhaa nchini.

## 9.0. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 – MACHI, 2024

**60. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipanga kutumia **Shilingi Bilioni 28. 41** kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi bilioni 26.01** kwa ajili ya mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Park) na **Shilingi bilioni 2.40** kwa ajili ya mradi wa kuendeleza

Uwanja wa Maonesho ya Kimataifa Dimani. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 9.0.1. Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Parks)

61. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuanzisha maeneo tengefu ya viwanda kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kutengeneza bidhaa za viwandani , kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuongeza mauzo ya nje. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mradi huu ulipangiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 26.01**. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) mradi ulipangiwa jumla ya **shilingi Bilioni 25.46,** hadi kufikia Machi 2024, mradi huu umeingiziwa jumla ya **Shilingi Bilioni 6.07** sawa na asilimia 24 ya makadirio kwa mwaka. Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

   i. Wizara imekamilisha kazi ya uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya ardhi (Master Plan) ya eneo la Viwanda Dunga na Chamanangwe kupitia kampuni ya CRM Land Consult (T) Limited ambayo Wizara iliingia makubaliano nayo ya kufanya kazi hiyo kwa gharama ya **Shilingi Milioni 577.846** pamoja na VAT.

   ii. Katika kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara ya mzunguko na barabara za ndani katika eneo la Viwanda Dunga.

Wizara chini ya Mkandarasi, China Civil Engineering Construction Corporation – CCECC inaendelea na ujenzi huo kwa urefu wa kilomita 7.83 kwa kiwango cha lami kwa thamani ya **Shilingi Bilioni 23.36** pamoja na VAT. Hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni asilimia 50 ambapo barabara zote zimekamilika kwa kiwango cha kifusi.

iii. Ujenzi wa Miundombinu ya maji katika eneo la Viwanda Dunga unaendelea kupitia Mkandarasi wa Kampuni ya Simba Developer Ltd ambao unajumuisha mnara wa tangi la maji lenye ujazo wa lita milioni moja, uchimbaji wa visima vitatu (3) na utandazaji wa bomba za maji kwenye eneo lote la Viwanda lenye ukubwa wa ekari 173 kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 3.46** pamoja na VAT. Kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 46 ambapo kisima kimoja kimekamilika na ujenzi wa 'base' ya chini na ya kati wa tangi umekamilika.

iv. Kazi zote za ujenzi wa miundombinu ya maji pamoja na barabara katika eneo hilo la Dunga unasimamiwa na Mshauri elekezi, Kampuni ya MS/Nimeta Consult (T) kwa gharama ya **Shilingi Milioni 652.26** pamoja na VAT.

### 9.0.2. Mradi wa Kuyaendeleza Maeneo ya Maonesho ya Biashara Dimani.

**62. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa kuweka eneo la kisasa kwa ajili ya maonesho ya Kimataifa Zanzibar ambapo umejenga ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua zaidi ya watu 1,500. Eneo hili pia lina uwezo wa kuchukua washiriki wa maonyesho wastani wa watu 650 pamoja watembeaji wastani wa watu 8,000. Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni 2.40** na hadi kufikia Machi, 2024 mradi huu umeingiziwa jumla ya **Shilingi Bilioni 7.75.** Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi – JKU imekamilisha ujenzi wa miundombinu katika eneo la maonesho, ambayo ni ukuta wa uzio, vikuta vya kufunga mashamiana, uwekaji sawa wa eneo, maegesho ya vyombo vya moto pamoja na vyoo. Ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 80. Hatua inayoendelea ni kumalizia ujenzi wa uwanja pamoja na ujenzi wa jengo la utawala.

ii. Wizara imekamilisha ununuzi wa vifaa vya maonesho yakiwemo mashamiana makubwa,

vifaa vya kujengea vibanda vya kuoneshea bidhaa, vifaa vya umeme, genereta, viti pamoja na meza. Vifaa hivyo, tayari vimefungwa katika eneo husika na vimeanza kutumika katika Tamasha la 10 la Biashara katika maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi na Tamasha la Muungano lililofanyika Aprili, 2024. Vile vile, Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar imefanikisha upatikanaji wa huduma ya umeme katika eneo la maonesho kwa kuweka waya wa njia kubwa na ndogo pamoja na transfoma.

### 9.0.3. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango (ZBS): Wizara kupitia ZBS imeendelea na utekelezaji wa mradi kwa kuendelea na ununuzi wa vifaa vya maabara pamoja na ujenzi wa maabara. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 ZBS iliweza kutekeleza mradi huo kama yafuatavyo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa jengo la ukaguzi wa vyombo vya moto na Kituo jumuishi.
ii. Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Maabara ya Ugezi katika eneo la Maruhubi pamoja na utanuzi wa Maabara ya Vimelea na Kemikali.

iii. Ununuzi wa vifaa vya Maabara ya Ugezi.
iv. Ununuzi wa vifaa vya mashine ya kupimia gesi ya Maabara.
v. Ununuzi wa mitambo ya ukaguzi wa vifaa vya moto
vi. Ununuzi na uwekaji wa Lifti kwa ajili ya jengo la Ofisi Maruhubi.

**64. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 mradi huu ulipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.65** hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **Shilingi milioni 557.23** zimetumika sawa na asilimia 19.13.

### 9.0.4. Programu ya Kuimarisha Wajasiriamali kupitia Huduma za Maendeleo ya Biashara (BDS) na Kuboresha Ubora na Uzalishaji (KAIZEN)

**65. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuongeza tija katika uzalishaji viwandani (Kaizen) na kuimarisha ufanisi na ubora wa huduma kwa watoa huduma za biashara Business Development Service (BDS). Katika kutekeleza programu hii, Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japani imeingia makubaliano ya utekelezaji kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani (JICA).

66. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ni ya miaka minne kuanzia Juni, 2023 hadi Mei, 2027 na inatekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa upande wa Tanzania Bara na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Zanzibar. Utekelezaji wa Programu hii Kwa upande wa Zanzibar ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imetoa mafunzo ya wakufunzi (Kaizen Trainers) kwa washiriki 21(wanawake 11 na wanaume 10) wakiwemo watumishi wa Serikali pamoja na wafanyakazi wa viwandani. Aidha, jumla ya washiriki sita (6) (wanawake 4 na wanaume 2) walipatiwa vyeti baada ya kufikia vigezo vyote vya kuwa wakufunzi na 15 (wanawake 7 na wanaume 8) wanaendelea ili kukamilisha vigezo vilivyowekwa.

ii. Kukamilika kwa zoezi la kutembelea na kuvipitisha Viwanda kwa ajili ya mafunzo ya kivitendo. Jumla ya viwanda sita (6) ndivyo vimechaguliwa. Sambamba na zoezi hilo, Viwanda vilivyokamilisha utekelezaji wa mafunzo ni pamoja na Zanto company, Lootah Group of Company na Inaya Cosmetics ambapo pia vilipatiwa vyeti maalum. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi utendelea kutoa mafunzo ya wakufunzi ya BDS na Kaizen kwa Unguja na Pemba.

## 10.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI AMBAZO HAZIPOKEI RUZUKU SERIKALINI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024.

### 10.0.1. Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)

67. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ZBS ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 6.96 kwa ajili ya kutekeleza kazi zake kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 3.94 kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi bilioni 3.016 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 ZBS imeingiziwa jumla ya **Shilingi bilioni 3.22** sawa na asilimia 46.3. Aidha, ZBS ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi bilioni 7.0** kutokana na vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia Machi, 2024 imeweza kukusanya **Shilingi bilioni 6.65** sawa na asilimia 95.

68. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 ZBS imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

   i. ZBS kupitia kiwango cha Kimataifa cha upimaji katika maabara ISO/IEC 17025:2017 imefanikiwa kupata ithibati (Accreditation) ya maabara ya mafuta na nishati;

ii. ZBS imeandaa viwango 90 kwa mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 100 ya lengo la kuandaa viwango 90. Aidha ZBS, imefanikiwa kuuza viwango 61 sawa na asilimia 102 ya uuzaji wa viwango 60 vilivyotarajiwa;

iii. Jumla ya Shehena 957 za bidhaa nyengine (General goods) zimekaguliwa na kupewa vyeti sawa na asilimia 95.7 ya utekelezaji ukilinganishwa na jumla ya shehena 1,000 zilizotarajiwa kutolewa na Mawakala wa Ukaguzi nje ya nchi kupitia Mfumo wa PvoC;

iv. Ukaguzi wa bidhaa mbali mbali ( General goods) kupitia Mfumo wa ukaguzi ndani ya nchi (DI) ulifanyika na jumla ya Kontena 6,148 za Futi (40) zilikaguliwa na kontena 5,321 za Futi (20) zilikaguliwa. Kwa upande wa ukaguzi wa vyombo vya moto jumla ya gari 5,578 na pikipiki 5,096 zimekaguliwa baada ya kuingia nchini na kaguzi 42 za masokoni zimefanyika . Aidha, ukaguzi wa mafuta ya Nishati kupitia mfumo wa (DI) umefanyika ambapo lita 190,890,242 na shehena za bidhaa (General Goods) 5,272 zimekaguliwa katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar;

v. ZBS imepokea jumla ya sampuli 768 sawa na asilimia 82 ya shabaha ya upokeaji sampuli 936. Aidha, bidhaa 68 kati ya 766 zilizofanyiwa uchunguzi wa kimaabara hazikukidhi matakwa ya viwango husika;

vi. ZBS imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa magari na pikipiki katika eneo lililopo mkabala na Ofisi za ZBS Maruhubi ambacho kina uwezo wa kukagua vyombo vya moto 300 kwa siku;

vii. Katika utekelezaji wa kazi za uandaaji wa viwango ZBS imeshiriki katika mikutano inayohusiana na uandaaji wa viwango vya Kitaifa katika maeneo ya Arusha, Morogoro, Dar es-salam na Zanzibar. Kwa upande wa uandaaji wa viwango Kikanda na Kimataifa ZBS imeshiriki mikutano nchi za Botswana, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Ghana yenye lengo la kuhakikisha matakwa ya wadau wa Zanzibar yanawasilishwa na kujumuishwa ipasavyo;

viii. Vyeti 18 vya alama ya ubora ZBS vimetolewa kwa kutumia Kiwango cha Zanzibar (ZBS Quality Mark) na vyeti 27 vimehuishwa baada ya kumaliza muda wake wa matumizi sawa na asilimia 90 ya makadirio ya vyeti 30; na

ix. ZBS imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi watano (5) wakiwemo (wanawake 2 na wanaume 3) katika fani ya ***food science, Enviromental Study, food quality and Safety Assurance, Economic and Finance*** na Master in Food Science. Aidha, Wafanyakazi 98 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya kuhamasisha jamii juu ya huduma za ZBS.

### 10.0.2. Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar (BPRA)

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 BPRA ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 1.4** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia Machi, 2024 imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 1.3** sawa na asilimia 92. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 350.50** ziliingizwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi milioni 641.73** ziliingizwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, BPRA ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi bilioni 1.43** hadi kufikia Machi 2024, BPRA imeweza kukusanya **Shilingi milioni 1.93** sawa na asilimia 135 ya makadirio. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa usajili wa Makampuni na Tozo ya stamps.

**70. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 BPRA imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. BPRA imefanya usajili wa Kampuni 1,059, Majina ya Biashara 1,491, Alama za Biashara 1,328 na Nyaraka 934;

ii. Wizara kupitia BPRA imefanya mapitio ya Sheria na Kanuni zinazosimamiwa na BPRA kwa Sheria ya Kampuni na kupatikana kwa Rasimu ya awali, Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, kuandaa Kanuni ya Sheria ya Mmiliki Mnufaika (pamoja na kufanya mapitio ya Tozo zote za usajili na kupata Rasimu ya awali;

iii. Wakala umetoa uelewa kwa wafanyabiashara na vikundi vya Wajasiriamali katika masuala ya urasimishaji, usajili na taratibu nyingine za kibiashara kupitia vipindi vya Televisheni na Redio;

iv. BPRA imeratibu vikao vitatu (3 ) ambavyo ni Kikao cha Urasimishaji wa Kazi za Mali Bunifu na Biashara kwa wafanyabiashara, Kikao cha uwasilishaji wa Sheria ya Ofisi ya BPRA na Kikao cha kuwasilisha Mpango Mkakati wa BPRA kwa Wadau;

v. Wizara kupitia BPRA imeshiriki mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na mafunzo ya vitendo kuhusu maswali ya Malibunifu nchini Spain, Mfumo wa Usajili wa Malibunifu nchini Botswana na kuhudhuria mafunzo ya kuongeza uelewa juu ya kutangaza matokeo ya Kikanda kwa kutumia njia mbali mbali za mawasiliano kwa kuitangaza dhana ya Malibunifu; na

vi. Jumla ya Wafanyakazi watatu (3) (wanawake 2 na mwanamme 1) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Mawasiliano, Manunuzi, Rasilimali Watu na wafanyakazi sita (6) (wanaume 3 na wanawake 3) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Sheria za Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na mafunzo ya kujitayarisha na kustaafu.

### 10.0.3. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)

**71. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika (Corporate Strategic Plan) wa miaka mitatu 2023-2025 pamoja na Mpango wa Biashara wa miaka mitano 2021-2025.

72. **Mheshimiwa Spika,** Shirika liliendelea kuimarisha Majengo kwa lengo la kuongeza mapato na kuhuisha ustawi wa Shirika. Aidha, Shirika limeendelea kuhakikisha mashirikiano na Wadau wa zao la karafuu na bidhaa nyengine yanaimarishwa. Kwa mwaka 2023/2024 Shirika lilikabiliwa na msimu wa wastani wa vuno la karafuu.

73. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Shirika lilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 12.1** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 Shirika limetumia jumla ya **Shilingi bilioni 7.6** sawa na asilimia 62.8 ya makadirio kwa miezi tisa. Aidha, Shirika lilipanga kukusanya mapato ya **Shilingi bilioni 84.5** kutokana na vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia Machi, 2024 Shirika limeweza kukusanya **Shilingi bilioni 65.5** sawa na asilimia 77.

74. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Shirika limefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

    i. Shirika katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2024 lilikadiria kununua tani 4,380 za karafuu kavu kwa gharama ya Shilingi 60.4 bilioni. Hadi kufikia Machi 2024, Shirika

limeweza kununua tani 3,298.8 za karafuu kavu kutoka kwa Wakulima kwa gharama ya Shilingi 47.5 bilioni. Karafuu zilizonunuliwa ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka mzima. Shirika limenunua kilo moja ya karafuu kwa bei ya 15,000 kwa daraja la kwanza, daraja pili Shilingi 13,500 , daraja la tatu Shilingi 12,500 na mpeta Shilingi 7,000 kutoka kwa mwananchi.

ii. Shirika lilikadiria kununua jumla ya tani 786 za makonyo kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.17. Hadi kufikia Machi 2024, Shirika limenunua jumla ya tani 627.6 za makonyo kwa gharama ya Shilingi milioni 941.4 sawa na asilimia 79.8 ya makadirio kwa miezi tisa. Aidha, manunuzi ya karafuu pamoja na makonyo yamepungua kutokana na msimu kuwa mdogo kinyume na matarajio.

iii. Shirika limefanikiwa kuuza karafuu nje ya nchi kwa bei ya Dola za Kimarekani 8,500 kwa tani moja FOB Zanzibar na makonyo yameuzwa kwa bei ya Dola za Kimarekani 850 kwa tani moja FOB Zanzibar. Aidha, Shirika limeweza kuuza nje ya nchi jumla ya tani 3,190 za karafuu na makonyo tani 694.

iv. Shirika liliingia makubaliano na kiwanda cha kuzalisha Sukari Mahonda ya kununua

jumla ya tani 3,000 za sukari kwa gharama ya Shilingi bilioni 6.6. Hadi sasa Shirika limeshalipia fedha za Sukari tani 1,500 kwa gharama ya Shilingi bilioni 3.3 na jumla ya tani 1,420 zimeshasambazwa kwa Waagizishaji na kuuzwa kwa wananchi.

v. Katika kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mimea Shirika limefanya ununuzi wa vinu viwili vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 85,000 kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya mimea ambapo vinu hivyo vinatarajiwa kuwasili katika robo ya nne ya mwaka huu.

vi. Jumla ya wafanyakazi watano (5) (wanawake 2 na wanaume 3) wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya Uzamili katika fani za Usimamizi wa Biashara, Biashara za Kimataifa na Uchumi na Fedha. Wafanyakazi wawili (mwanamke1 na mwanaume1) wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika fani ya Uchumi na Ufundi Umeme. Aidha, wafanyakazi 15 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

### 10.0.4. Kampuni ya Mwani Zanzibar ( ZASCO)

**75. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kampuni ilipangiwa jumla ya

**Shilingi bilioni 5.3** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia Machi, 2024 imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 1.7** sawa na asilimia 32 ya makadirio kwa miezi tisa. Aidha, Kampuni ilipangiwa kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 4.8 kutokana na vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia Machi, 2024 Kampuni imeweza kukusanya **Shilingi milioni 786.6** sawa na asilimia 16.5 ya makadirio ya miezi tisa. Hali hii imetokana na ukosefu wa mtaji wa kununulia mwani.

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Kampuni imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kampuni imekamilisha utiaji saini wa mkataba wa uendeshaji na usimamizi wa kiwanda cha kusarifu zao la mwani na Kampuni ya Nutri-san. Aidha, Kampuni hiyo inaendelea na mchakato wa kutafuta mashine ambazo zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwaka 2024.

ii. Kampuni imeendelea kufanya biashara ya mwani aina ya Ulva, hadi kufikia Machi, 2024, Kampuni imefanikiwa kununua wastani wa tani 724.8 za mwani aina ya Ulva. Mwani huo ulinunuliwa kwa gharama ya Shilingi milioni

779.8 na kuuza tani 575 kwa Shilingi milioni 786.6.

iii. Kampuni imenunua mwani aina ya Ulva kwa Shilingi 800 kwa kilo, mwani aina ya Spinosum Shilingi 1,000 kwa kilo na mwani aina ya Cottonii Shilingi 2,100 kwa kilo kutoka kwa mwananchi.

iv. Kampuni imetoa kamba za kulimia mwani zenye upana wa milimita 1, 4 na 10 kwa vikundi 222 (vikundi 147 Pemba na 75 Unguja) vya wakulima wa Mwani ili kusaidia katika kuendelea na uzalishaji wa zao hilo.

v. Wafanyakazi 12 wa Kampuni wamepatiwa mafunzo juu ya "Risk management" na Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali Chakavu. Aidha, wafanyakazi wawili (2) walipatiwa mafunzo juu ya mfumo wa kufunga Hesabu na Ukarani.

## 11.0. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 11.0.1. Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2024/2025

77. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutayarisha bajeti ya mwaka 2024/25, Wizara imezingatia

nyenzo muhimu ambazo ni Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Hotuba na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ushauri wa Baraza la Wawakilishi na Miongozo mbalimbali ya Kisera na Kisheria inayosimamiwa na Wizara.

78. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza vipaumbele katika maeneo makuu matatu (3) ambayo yanalenga kuimarisha Sekta ya viwanda, kuimarisha Biashara na kutafuta Masoko pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na utoaji huduma. Maeneo hayo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

**Sekta ya Viwanda**

79. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza sekta ya viwanda, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda Dunga, Chamanangwe na Pangatupu. Kwa upande wa Dunga na Chamanangwe Wizara inatarajia

kuweka miundombinu ya majengo ya viwanda, maji , umeme pamoja na barabara za ndani. Aidha, upande wa Pangatupu Wizara imepanga kufanya upimaji wa udongo na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi.

ii. Kuanzisha mfumo wa usajili wa takwimu za viwanda. Mfumo huo utatumika kwa ajili ya kukusanya takwimu na kutoa ripoti zinazohusiana na mwenendo mzima wa Viwanda kwa upande wa Zanzibar na utajumuisha kwa pamoja na mfumo wa BPRA na BRELLA.

## Kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko

**80. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuendeleza Ujenzi kwenye eneo la maonesho ya kibiashara Dimani: Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kuendelea kuimarisha miundombinu tofauti ikiwemo kuweka miundombinu ya maji ya uhakika katika eneo lote la kituo, kufunga kamera za CCTV na ‘scanner, ununuzi wa vifaa na kuweka mifumo ya usajili wa washiriki na kuendelea na ujenzi wa jengo la Utawala.

ii. Kuratibu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre): Wizara itaendelea na juhudi za kutafuta Wawekezaji wenye masharti nafuu ili kushirikiana katika ujenzi wa kituo hiki.

**Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma**

**81. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Mazingira ya ufanyaji Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kufanya ukaguzi na uchunguzi wa bidhaa, bei elekezi ya bidhaa na bidhaa bandia na kuweka mikakati kwa watumiaji pamoja na kusikiliza mashauri ya kumlinda mtumiaji;

ii. Kufanya uchunguzi na kusikiliza mashauri yanayoathiri ushindani katika soko la miungano ya Makampuni;

iii. Kufanya utafiti juu ya athari za kijamii na kiuchumi zinazotokana na matumizi ya bidhaa bandia;

iv. Kufanya tafiti juu ya athari za miungano ya makampuni isiyorasimishwa na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara;

v. Kufanya matengenezo ya jengo linalotarajiwa kutumiwa na Ofisi za Baraza la Ushindani Halali wa Biashara;

vi. Kupitia na kupendekeza marekebisho ya Sheria 20 za Mamlaka za Utoaji leseni Zanzibar;

vii. Kufanya ujenzi wa ofisi ya Mamlaka za Utoaji leseni;

viii. Kufanya Tafiti katika masuala ya Biashara na Viwanda ambayo italenga katika maeneo ya biashara ya mtandao ili kuweza kubaini utayari wa mazingira ya ufanyaji biashara za kimtandao kwa Zanzibar;

ix. Kuratibu utekelezaji wa yatokanayo na Ripoti ya Tathmini ya Mazingira ya ufanyaji Biashara Zanzibar (Zanzibar Blueprint) kwa lengo la kuimarisha mazingira bora ya biashara;

x. Kufanya mikutano ya Mabaraza ya Biashara na Jukwaaa la Biashara;

xi. Kuratibu utungwaji wa Sheria ya Maendeleo ya Sekta binafsi;

xii. Uanzishaji wa Mifumo ya Kielektroniki katika Usajili, Ukusanyaji na Ugawaji wa Mirabaha (Registration, Licensing and Royality Distribution Systems); na

xiii. Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki (Namba 14) ya mwaka 2003 na kuandaa Kanuni mbali mbali za Hakimiliki.

xiv. Kufanya tasnia ya hakimiliki kuwa biashara (Commercialization of Copyright Industry).

**Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA)**

**82. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imepanga kufanya mapitio ya Sheria za BPRA kwa lengo la kuimarisha mazingira bora ya ufanyaji Biashara.

ii. Kutoa uelewa kwa wafanyabiashara na vikundi vya wajasiriamali katika masuala ya urasimishaji, usajili na taratibu nyingine za kibiashara kwa Mikoa yote ya Unguja na Pemba.

**Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)**

**83. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza Taasisi ya Viwango, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Uimarishaji wa Taasisi kwa kupata Ithibati

(Accreditation) ya Maabara mbili (2), Maabara ya chakula ya Mikrobiolojia na Maabara ya Umeme.

ii. Kuimarisha huduma za udhibiti ubora ndani ya Taasisi kwa upande wa Pemba kwa kujenga Ofisi pamoja na Maabara.

iii. Kutoa uelewa na uhamasishaji kwa wajasiriamali na wazalishaji kupata Alama ya Ubora ya ZBS.

**Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)**

**84. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuanzisha Viwanda viwili vipya vya uzalishaji wa mafuta ya mimea vyenye uwezo wa kuchukua kilo 350 za majani kwa wakati mmoja ambazo zitakuwa na uwezo wa kuzalisha wastani wa lita sita (6) za mafuta.

ii. Uzalishaji wa Vifungashio vya Bidhaa mbali mbali hasa bidhaa za karafuu na mazao mengine ya kilimo.

iii. Kutanua wigo wa Biashara zinazoendeshwa na Shirika kwa kuanza kufanya biashara ya Bidhaa za Vyakula muhimu hapa Zanzibar.

iv. Kufanya ununuzi wa tani 5,000 za karafuu.

**Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO)**

85. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kampuni ya Mwani itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

    i. Kuanza uzalishaji katika Kiwanda cha kusarifu mwani Chamanangwe Pemba.

    ii. Kuimarisha uwezo wa wakulima juu ya kuandaa mwani baada ya uvunaji.

## 12.0. MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025

86. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2024/25 imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 60.28.** Kati ya fedha hizo jumla **Shilingi bilioni 1.68** kwa Matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi bilioni 3.13** kwa malipo ya mishahara. Aidha, **Shilingi bilioni 50.32** zimetengwa kwa kazi za Maendeleo kwa Programu ya kuendeleza maeneo ya Viwanda na Mazingira Bora ya Biashara. Aidha, Wizara imepangiwa ruzuku ya **Shilingi bilioni 5.15.**

87. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda itatekeleza Programu Kuu tatu (3). Programu kuu hizo ni programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; Programu ya Maendeleo

ya Viwanda na Ujasiriamali; na Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara.

88. **Mheshimiwa Spika,** Katika programu kuu ya kwanza ambayo ni Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; imegawika katika Programu ndogo tatu (3). Program hizo ni Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara kwa Pemba. Katika kutekeleza shughuli zake, programu hii imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 3.68.**

89. **Mheshimiwa Spika,** Katika Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Katika kutekeleza majukumu yake programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 1.49**.

90. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la uandaaji na uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda. Katika kutekeleza majukumu yake programu hii imepangiwa **Shilingi milioni 542.03.**

91. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo inaratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya S**hilingi bilioni 1.64.**

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya pili ambayo ni Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali imegawika katika Programu ndogo mbili. Program hizo ndogo ni Ukuzaji Viwanda na Maendeleo ya Ujasiriamali. Katika kutekeleza shughuli za programu hii imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 40.75.**

93. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda ina jukumu la kutoa huduma ya uimarishaji wa Sekta ya Viwanda, Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's na Ukuzaji wa MSME's. Ili kutekeleza majukumu yake programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 40.71**.

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ambayo ina jukumu la kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali ili kutekeleza programu hii ndogo imepangiwa **Shilingi millioni 33.55**

95. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya tatu ni

Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Programu hii imegawika katika Programu ndogo tatu (3) ambazo ni Ukuzaji masoko na usafirishaji; uwezeshaji biashara na utengamano wa kibiashara. Ili kutekeleza huduma zilizopangwa katika Programu kuu hii kwa mwaka 2024/2025, imepangiwa jumla ya Shilingi bilioni 15.84.

96. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji ina jukumu la kutoa huduma ya kuongeza fursa za masoko kwa bidhaa za Zanzibar pamoja na urahisishaji biashara. Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji imepangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 10.54.**

97. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara yenye jukumu la kuimarisha mazingira mazuri ya biashara ambayo inatekelezwa na Idara ya Biashara, pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ambazo ni ZFCC, BLRC, ZAWEMA, COSOZA, ZNBC na ZFCT. Ili kutekeleza jukumu lake kupitia programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 5.24.**

98. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara wenye jukumu la kuimarisha biashara huria inayopelekea

upanuzi wa soko na kuongeza biashara baina ya nchi na nchi itasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza shughuli zilizopangwa programu hii ndogo imepangiwa jumla ya **Shilingi milioni 43.84.**

## 13.0. MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 13.0.1. Mapato ya Serikali

**99. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara yangu imepangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi billioni 1.93** ukilinganisha na makusanyo ya mwaka 2023/2024 ya **Shilingi Bilioni 1.75.** Hii imesababishwa na maamuzi ya Serikali kuhamishia majukumu ya Taasisi ya Hakimiliki Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio kama inavyoonekana katika **Jadweli Namba 1.**

**Jadweli Namba 1:** ***Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024-2025***

| KIFUNGU | MAELEZO | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **564,000,000** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 564,000,000 |
| | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **958,000,000** |
| 1422077 | Malipo ya kazi za Biashara | 958,000,000 |
| | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **14,000,000** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 14,000,000 |
| | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRC)** | **50,140,000** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa Mamlaka za Leseni | 50,140,000 |
| | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **99,933,000** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 99,933,000 |
| | | |
| **R0101** | **Afisi kuu Pemba** | **49,717,000** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 39,717,000 |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 10,000,000 |
| | | |
| **R0114** | **Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki** | **200,062,000** |
| 1422117 | Mapato ya usajili na ada ya Mwaka | 200,062,000 |
| **JUMLA** | | **1,935,852,000** |

## 13.0.2.Matumizi

100. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2024/25 imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 60.28.** Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 50.32** zimepangwa kwa ajili ya kazi za Maendeleo, **Shilingi bilioni 1.67** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi bilioni 3.13** kwa ajili ya mishahara. Aidha, **Shilingi**

**bilioni 5.14** zimepangwa kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kwa Taasisi za Wizara. Mchanganuo wa matumzi hayo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali nambari 2.**

***Jadweli Namba 2: Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2024/2025***

| FUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | Makadirio |
|---|---|---|
| PR0101 | Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biasharara na Maendeleo ya Viwanda | 3,686,696,000 |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 1,498,953,000 |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara | 542,033,000 |
| SR010103 | Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 1,645,710,000 |
| | | |
| PR0102 | Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali | 40,752,650,000 |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 40,719,098,000 |
| SR010202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 33,552,000 |
| | | |
| PR0103 | Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara | 15,841,654,000 |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 10,549,441,000 |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 5,248,373,000 |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 43,840,000 |
| **JUMLA YA KIFUNGU RO1** | | **60,281,000,000** |

## 14.0. HITIMISHO

101. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia maelezo ya Hotubu hii napenda kukushukuru tena wewe binafsi,Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Utalii, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kutupatia maoni na ushauri pamoja na mashirikiano wanayotupatia ambayo yametusaidia kwa kiasi kikubwa kuleta maendeleo katika Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini.

102. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa wale wote walioshirikiana nasi kufanikisha malengo ya Wizara katika kipindi cha mwaka 2023/2024 miongoni mwao ni Trade Mark Africa (TMA), Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) Shirika la Malibunifu Duniani (WIPO), TANTRADE, Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya NMB, Benki Kuu ya Tanzania, Benki ya Azania, Jumuiya ya Wafanyabiashara (ZNCC), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC),Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), STAMICO, ZICTIA, TRA, ZSTC, ASAS, Air Tanzania, TTCL, Tigo/

Zantel na Wafanyabiashara na Wajasiriamali mbali mbali waliosaidia kufanikisha Tamasha la biashara la 10 lililofanyika kwa mara ya kwanza katika eneo lake la kudumu katika viwanja vya maonyesho Dimani.

**103.** **Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda niwashuruku Viongozi wenzangu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda nikianza na Katibu Mkuu Ndugu Fatma Mabrouk Khamis, Naibu Katibu Mkuu Dkt Said Seif Mzee, Wakuu wa Taasisi wote, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa mashirikiano yao wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ni matarajio yangu kwamba mashirikiano hayo yataendelezwa kwa ufanisi zaidi katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

**104.** **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya taarifa hii naomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kupokea, kujadili na hatimae kuikubali taarifa hii ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 na kuidhinisha makadirio ya Shilingi bilioni 60.28 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN**

**WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

**Kiambatanisho Nambari 1:**

**Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu katika Soko la Zanzibar katika kipindi cha Julai- Machi, 2023/2024.**

| BIDHAA/TANI | Bidhaa (Tani) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mchele** | **Sukari** | **Unga wa ngano** | **Mafuta ya Kula** |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka nje ya nchi | 80,843 | 15,067 | 1,643 | 96,750 |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka Tanzania Bara | 3,918 | 0 | 2,863 | 0 |
| Bidhaa zilizozalishwa nchini | 0 | 4,560 | 38,482 | 0 |
| **Jumla ya Bidhaa** | **84,761** | **19,627** | **42,988** | **96,750** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2024***

**Kiambatanisho Nambari 2:**
**Wastani wa Bei za Reja Reja (Kg) kwa Bidhaa Muhimu Katika Soko la Zanzibar, 2023/2024.**

| BIDHAA/BEI | Wastani wa Bei za Reja Reja (Tshs/Kg) | | |
|---|---|---|---|
| | **Julai-Septemba** | **Oktoba-Disemba** | **Januari-Machi** |
| Mchele wa Basmati | 4,000 - 4,500 | 4,000 - 4,500 | 4,000- 4,500 |
| Mchele aina nyengine | 2000 - 2,500 | 2,200 - 2,500 | 1,800- 2,500 |
| Mchele wa Mbeya | 2,800 - 4,600 | 2,600 - 4,000 | 2,600- 4,000 |
| Unga wa ngano | 1,800 - 2,000 | 1,800 - 2,000 | 1,800-2,000 |
| Sukari | 2500-2,600 | 2,900- 3,000 | 3,000- 3,200 |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2024***

**Kiambatanisho Nambari 3:**

**Mapato ya Wizara kwa kipindi cha Miezi Tisa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Kifungu | Maelezo | Makadirio kwa Mwaka 2023/24 | Makadirio kwa Miezi Tisa 2023/24 | Makusanyo kwa Miezi Tisa 2023/24 | Asilimia ya Makusanyo Kwa miezi Tisa |
|---|---|---|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **563,644,000** | **441,278,000** | **252,750,925** | **57%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 563,644,000 | 441,278,000 | 252,750,925 | 57% |
| | | | | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **957,850,000** | **698,940,000** | **378,865,000** | **54%** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 957,850,000 | 698,940,000 | 378,865,000 | 54% |
| | | | | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **16,896,000** | **12,326,000** | **17,400,000** | **141%** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 16,896,000 | 12,326,000 | 17,400,000 | 141% |
| | | | | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRC)** | **63,953,000** | **57,521,000** | **49,020,000** | **85%** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa Mamlaka za Leseni | 63,953,000 | 57,521,000 | 49,020,000 | 85% |
| | | | | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **99,933,000** | **57,436,000** | **49,440,210** | **86%** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 99,933,000 | 57,436,000 | 49,440,210 | 86% |
| | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **47,724,000** | **37,448,500** | **41,615,654** | **111%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 39,717,000 | 31,845,000 | 29,175,654 | 92% |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 8,007,000 | 5,603,500 | 12,440,000 | 222% |
| **Jumla Kuu** | | **1,750,000,000** | **1,304,949,500** | **789,091,789** | **60%** |
| | Mapato Mengineyo (Maonesho) | | - | 314,244,057 | |
| | **Jumla Kuu** | **1,750,000,000** | **1,304,949,500** | **1,103,335,846** | **85%** |

**Kiambatanisho Nambari 4**

**Mchanganuo wa matumizi ya fedha kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi), 2023/2024**

| KIFUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | KIASI KILICHOPANGWA KWA MWAKA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA MIEZI TISA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPATIKANA MIEZI TISA | ASILIMIA YA KILICHOPATIKANA |
|---|---|---|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na uratibu wa Wizara BMV** | **4,053,415,640** | **3,002,563,232** | **2,325,209,164** | **77%** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 2,575,533,637 | 1,862,486,232 | 1,405,078,535 | 75% |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara | 570,498,500 | 446,886,750 | 286,181,001 | 64% |
| SR010103 | Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 907,383,503 | 693,190,250 | 633,949,628 | 91% |
| | | | | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **27,291,144,360** | **26,479,741,620** | **6,721,157,743** | **25%** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 26,393,724,360 | 25,748,895,620 | 6,539,040,343 | 25% |
| SR010202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 897,420,000 | 730,846,000 | 182,117,400 | 25% |

| KIFUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | KIASI KILICHOPANGWA KWA MWAKA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA MIEZI TISA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPATIKANA MIEZI TISA | ASILIMIA YA KILICHOPATIKANA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **6,068,640,000** | **5,267,587,265** | **10,401,420,571** | **197%** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 3,806,374,000 | 3,425,774,000 | 9,261,266,389 | 270% |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 2,222,346,000 | 1,812,233,265 | 1,138,580,862 | 63% |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 39,920,000 | 29,580,000 | 1,573,320 | 5% |
| **JUMLA YA FUNGU RO1** | | **37,413,200,000** | **34,749,892,117** | **19,447,787,478** | **56%** |